

Kwa Nini Unaamini?

Jana usiku baada ya kuwasili nyumbani, nikaketi, na nikawasha luninga. Nikaangalia matokeo ya mpira wa miguu, nilifurahishwa kuona Indy akicheza vizuri, walakini nilikasirishwa kuona Don McDonald akinishinda. Hivyo, nikaanza kuendelea kama kawaida yangu kwa kufungua chaneli za taarifa za habari, ili tu kuona kinachoendelea. Kwa mshangao, nilikuta Larry King akiwa anajianda kumuuliza swali Joel Osteen kuhusiana na imani yake. King akamuuliza, “Kwa nini unaamini?”. Nikawaza, jibu la swali hili litakuwa la kuvutia. Huyu ni muinjilisti mashuhuri nchini kwa njia ya luninga, akiwa anakaribia kujibu swali kwa nini mtu amwamini Kristo; Nikawaza, ehee..., naelekea kusikia jambo mahsusi. Anaelekea kueleza kiundani kwa nini kila mtu anatakiwa kumwamini Kristo. Ndipo Joel akafunua kinywa chake. Nami nikagundua kwa haraka, ingawaje ana jina sawa na nabii mkubwa katika Agano la Kale na ndiyo pekee wanachofanana hawa wawili. Kwa ufahamu wake wote, hekima na maandalizi aliyoyafanya kwa ajili ya usaili kama huu akajibu kwa kifupi (huu ni ufupisho) “kwa sababu baba aliamini.”

Nini??? Huyu ndiye “mtu bora wa Mungu” anaeleza kwa nini anaamini kwamba Kristo ni mwana wa Mungu? “Baba aliamini.” Hivyo, hakuamini kutokana na uchinguzi wake mwenyewe. Hakuamini kwa sababu asili inavuma kushuhudia kwamba Mungu yupo. Hakuamini kwa sababu ya unabii uliotimilizwa. Anaamini kwa sababu tu amekuwa ni tunda la mazingira ya baba yake. Joel ana bahati baba yake hakuwa muuza madawa ya kulevya, mlevi, kuwadi, au vinginevyo. Kwa sababu Joel alipangiwa kuwa kama alichofanya babaye.

Ndipo, nikashangaa jamani!!! Kama vijana au watu wa umri wa kati wangeulizwa swali kama hilo katika kusanyiko nililotumika, wangeweza kujibu vyema zaidi? Je miongoni mwa ndugu vijana walio wengi ni waumini kwa sababu tu baba alikuwa muumini, mama alikuwa muumini? Nikajifikiria mwenyewe, nina uhakika siko hivyo. Kwa hiyo, kwa nini unaamini?

Kwa upande wake Joel Osteen angalau alikuwa mkweli!! Alikiri kwamba yuko vile alivyo leo kwa sababu ni tunda la mazingira ya baba yake, na siyo vinginevyo. Vipi wewe?

Si haki nikawa nawauliza swali kama hili halafu mimi mwenyewe silijibu. Na jana usiku nililijibu! Niliketi pale pale na kujiuliza “Kwa nini ninaamini?” Kwanza, naweza kuwahakikishia kuwa si kwa sababu baba aliamini. Atakuwa wa kwanza kuwaambia kwamba kutokusema kwake kitu kwangu haikumaanisha kichuguu cha maharage. Na nina ushahidi, mnyororo wake uliokatika ni ushahidi wa miaka ya kubembeza mikanda kwa sababu tu sikukubaliana na neno alilokuwa amesema. Sasa, kwa nini naamini? Zifuatazo ni sababu:

- 1) Kwa sababu alijifunua kwangu katika neno, 1 Yohana 5:11-13 , akanifunulia “mambo yote yapasayo uzima na utauwa” ,2 Petro. 1:3.
- 2) Imani huja kwa kusikia, Warumi 10:17

- 3) Ninaamini kwa sababu ya ushahidi na shuhuda za kitabu hiki kilichosheheni ishara alizozitenda Yesu, ambazo zinathibitisha Uungu wake, Yohana 20:30-31
 - a. Ninaamini kwa sababu ya ushahidi uliopo katika maandiko, Waebrania 11:1
 - b. Ushahidi wa sheria ya chanzo na athari.
 - c. Ushahidi wa asili ya maadili.
 - d. Sheria madiliko ya kiumbo (thermodynamics).
 - e. Mauti, kuzikwa na ufufuo wa Bwana wetu.
 - f. Kuzaliwa kwa njia ya bikira.
- 4) Ninaamini kwa sababu mitndo huthibitisha kuwa ni lazima pawepo na mbunifu, Waebrania 11:3; Zaburi. 19:1; 97:6; 2 Petro. 3:5.
- 5) Ninaamini kwa sababu ya “mambo yasiyoonekana...tsngu kuumbwa ulimwengu,” huvuma kuoneysha kuwa Muumbaji yupo Warumi 1:20.
- 6) Ninaamini kwa sababu hajawahi kujiacha kamwe bila ushahidi, Matendo ya mitume 14:17.
- 7) Ninaamini kwa sababu Mungu anasema na sisi leo kwa njia ya “mng’ao wake wa utukufu,” Waebrania 1:1-3 I
- 8) Ninaamini kwamba ndani ya mwanadamu kuna kitu kinachotufanya tusichoke kusaka ukamilifu. Kitu hicho kiliwekwa ndani yetu kutufanya tumtafute. “tena ameiweka hiyo milele ndani ya mioyo yao” Mhubiri 3:11.
- 9) Ninaamini kwa sababu tu Biblia inatanabaisha kwamba Mungu yupo Mwanzo 1:1. Mungu hakuanza kwa kutoa hoja kwamba yupo. Bali anaeleza tu, kama jambo lililo wazi.
- 10) Tofauti na wengi, ninaamini, naweza na nimeukubali ushahidi wa mabaki, uvumbuzi, uvuvio, historia, Jiografia, sayansi, mshikamano wa maandiko, uhai hutokana na uhai (viumbe vilivyo hai huzaliana kwa jinsia yao, Mwanzo 1:20,24). Ushahidi huu mwingine mwingi unathitisha kwamba Biblia iko sahihi na siyo Darwin.

Kabla sijahitimisha, tafakari, tafakari hili, Kwa nini unaamini?